

PURA



Mamlaka ya Udhhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli



JARIDA

TOLEO NA.1

JUNI 2021

PURA, wadau kuongeza ushiriki wa wazawa sekta ya mafuta na gesi



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa akimkabidhi cheti cha ushiriki Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PURA Mhandisi Charles Sangweni, kwenye Maonyesho ya 4 ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Maonesho hayo yalifanyika katika viwanja vya Sheikh Amri Abeid jijini Arusha.

3 Dibaji

4 Kuhusu PURA

6 PURA yazindua Baraza la Wafanyakazi

8 PURA yaeleza fursa zilizopo kwenye mkondo wa juu wa petroli

12 PURA, wadau kuongeza ushiriki wa wazawa katika mkondo wa juu wa petroli

15 Waandishi wa Habari na Wahariri chachu ya uelewa wa shughuli za mkondo wa juu wa petroli kwa jamii

17 PURA katika mapinduzi ya kiuchumi

19 Wanafunzi, wanaenzi watembelea mitambo ya uzalishaji gesi asilia

Anuani

5 Mtaa wa Samora, S.L.P 11439, Dar es Salaam, Tanzania,

Simu: (+255 22 2117156/9), **Nukushi:** (+255 22 2120799),

Baruapepe: (dg@pura.go.tz), **Tovuti:** (www.pura.go.tz)

Barabara ya Kikuyu, PSSSF Ghorofa ya 4, S.L P 1980, Dodoma.

Simu: (+255654712100)



Wapendwa

wasomaji, shughuli hizo za Mkondo wa Juu wa Petroli.

Nikwafurahateletunakukaribisha kwenye toleo la kwanza la jarida kwanza la Mamlaka ya Udhhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA).

Tumeazimia kutumia zana hii kuwasiliana na umma juu ya mambo yote yanayohusu shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli zinazodhibitiwa na Mamlaka hii.

Toleo hili linaangazia shughuli anuwai ambazo zilifanyika kati ya mwezi Julai 2020 hadi Machi 2021. Pia linapitia maoni kutoka kwenye vyombo vya habari juu ya Mamlaka na jinsi inavyoweza kuleta maendeleo makubwa katika ukuzaji wa tasnia ndogo ya mafuta na gesi nchini.

Mfululizowamajaridaambayoyatatolewa tangu sasa pia utazingatia kuongeza ushiriki wa Watanzania katika uuzaji wa bidhaa na huduma mbalimbali kwenye

Hii ni kuhakikisha kuwa wazawa wanabaki kuwa kiini cha maendeleo ya uchumi wa nchi yetu kupitia matumizi sahihi ya rasilimali na fursa zinazopatikana katika tasnia ya mafuta na gesi asilia.

Jukumu moja la msingi la PURA ni kusimamianakudhibitishughuliMkondowa Juu wa Petroli kwa kuhakikisha Watanzania wanapewa kipaumbele kwenye kupata fursa zinazopatikana katika tasnia husika.

Ni matumaini yetu kwamba majarida haya yatakuwa daraja la mawasiliano kati ya Mamlaka na umma wa Watanzania ili kuleta kuchochea maendeleo yanayohitajika katika sekta ya mafuta na gesi nchini Tanzania.

Asante na karibu sana.

Mhandisi Charles Sangweni
Kaimu Mkurugenzi Mkuu

Uanzishwaji wa PURA na majukumu yake

Mamlaka ya Udhhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) iliundwa kupitia kifungu cha 11 cha Sheria ya Petroli ya Mwaka 2015. Majukumu makuu matatu ya PURA ni pamoja na kuishauri Serikali juu ya masuala yanayohusu Mkondo wa Juu wa Petroli katika utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini, kusimamia na kudhibiti shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli; na kusimamia shughuli zote za mradi wa kusindika gesi asilia kuwa kimiminika (Liquefied Natural Gas – LNG).

Katika jukumu lake la kuishauri serikali, PURA inawajibika kumshauri Waziri mwenye dhamana ya masuala ya mafuta na gesi kuhusu utoaji, uhuishaji, usimamishaji, na ufutaji wa leseni za utafutaji na uendelezaji, kuishauri Serikali kuhusu kunadi vitalu kwa ajili ya utafiti na utoaji wa leseni ya uwekezaji katika maeneo mapya yenye viashiria vya mafuta na gesi nchini na kuishauri Serikali kuhusu majadiliano ya mikataba mbalimbali ya mafuta na gesi nchini.

Kwenye jukumu lake la ukaguzi na usimamizi wa Shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli, PURA ina wajibu wa kudurusu na kupitisha Mpango Kazi na Bajeti za Makampuni ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi, kuhakiki gharama za utafutaji na uendelezaji wa mafuta na



Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PURA, Mhandisi Charles Sangweni akimwonesha Naibu Waziri wa Nishati Stephen Byabato hali za leseni za uchimbaji kwenye shughuli za mkondo wa juu wa petroli kwenye ramani maalumu inayoonesha shughuli hizo. Naibu Waziri Byabato alifanya ziara kwenye ofisi za PURA jijini Dar es Salaam mnamo Desemba 15, 2020. Picha na Janeth Mesomapya

gesi zinatozotekelezwa na Makampuni ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi (IOCs) na kukagua na kufanya tathmini ya utendaji kazi wa Makampuni katika shughuli za mkondo wa Juu wa Petroli;

Pia inasimamia na kutunza data za utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi, ina wajibika kuhamasisha ushiriki wa wazawa ikiwa ni pamoja na kusaidia kampuni za Kitanzania kushiriki kikamilifu katika shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli.

Jukumu la PURA la tatu ni kudhibiti shughuli za uendelezaji wa Mradi wa usindikaji gesi asilia (LNG) ikiwa ni pamoja na kukagua na kuhakiki gharama, mapato na matumizi kwenye Mradi wa LNG, kupitisha mpango wa uendelezaji, kutoa leseni za uchakataji wa gesi asilia kuwa kimiminika, usafirishaji wa gesi

na uchakataji kutoka kimiminika kwenda gesi na kusimamia shughuli za uendelezaji wa Mradi wa LNG.

Hali ya utafutaji wa mafuta na gesi asilia

Shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi nchini Tanzania zilianza mwaka 1952. Ugunduzi wa kwanza wa gesi asilia nchini ulifanyika mwaka 1974 katika maeneo ya kisiwa cha Songo Songo mkoani Lindi chini ya kampuni za Azienda Generali Italiana Petroli (AGIP) kwa kushirikiana na American Oil Company (AMOCO). Ugunduzi wa pili wa gesi asilia ulifanyika mwaka 1982 katika maeneo ya Mnazi Bay Mkoani Mtwara chini ya Kampuni ya AGIP.

Kutokana na kuongezeka kwa kazi za utafutaji wa mafuta

na gesi nchini hususani katika kina cha maji ya bahari ya Hindi, ugunduzi mkubwa wa gesi asilia ulifanyika kati ya mwaka 2010-2012. Kiasi cha gesi asilia kilichogundulika nchini katika maeneo ya nchi kavu na baharini hadi kufikia Februari 2020, ni futi za ujazo Trilioni 57.54.

Kati ya futi za ujazo Trilioni 57.54 za gesi zilizogundulika nchini, gesi iliyogundulika nchi kavu (onshore) ni futi za ujazo Trilioni 10.46 huku upande wa Bahari Kuu ni futi za ujazo Trilioni 47.08.

Hali ya mikataba ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia

Mikataba ya Utafutaji, Uzalishaji na Ugawanaji wa

Mapato (PSAs) ya mafuta na gesi asilia iliyopo nchini kwa ujumla inafikia kumi na moja (11), ambapo mikataba nane (8) kati ya hiyo ni ya maeneo yaliyopo nchi kavu (onshore) na mitatu (3) ni maeneo yaliyopo kwenye kina kirefu cha bahari (offshore).

Mikataba nane (8) kati ya 11 ikiwemo Kitalu na.1, Kitalu Na.2 Kitalu Na.4, Kitalu cha Ruvu, Kilosa-Kilombero, Rukwa Kusini, Nyuni na Mtwara, ipo katika hatua za utafutaji; ambapo mikataba mitatu (3) ikiwemo Mnazi Bay, Songo Songo na Kiliwani Kaskazini ipo katika hatua ya uzalishaji.

Hata hivyo kutokana na changamoto za kiufundi, uzalishaji katika Kitalu cha Kiliwani Kaskazini umesimama na hivyo kubaki na uzalishaji wa

gesi asilia katika vitalu vya Mnazi Bay na Songo Songo.

Hali ya uzalishaji wa gesi asilia nchini

Kufikia mwezi Januari 2021, uzalishaji wa gesi asilia kutoka visima vya Mnazi Bay ulikuwa wastani wa futi za ujazo Bilioni 2.39 kwa mwezi sawa na wastani wa futi za ujazo Milioni 74 kwa siku.

Ambapo uzalishaji wa gesi asilia kutoka visima vya Songo Songo ulikuwa wastani wa futi za ujazo Bilioni 3.038 kwa mwezi sawa na wastani wa futi za ujazo Milioni 98 kwa siku, na hivyo kupelekea jumla ya uzalishaji wa gesi asilia nchini kufikia wastani wa futi za ujazo Bilioni 5.428 kwa mwezi sawa na wastani wa futi za ujazo Milioni 172 kwa siku.



Bodi ya Wakurugenzi, baadhi ya viongozi kwenye Menejimenti na wafanyakazi wa PURA wakiwa katika picha ya pamoja.

PURA yazindua Baraza la Wafanyakazi

Na Janeth Mesomapyia

Mabaraza ya wafanyakazi yanaelezwa kuwa nyenzo muhimu katika kuboresha mazingira ya kazi baina ya mwajiri na mwajiriwa ili kujitea tija kwa mustakabali wa taasisi na watu binafsi katika taasisi husika.

Kutokana na umuhimu wake huo, Baraza la Wafanyakazi la Mamlaka ya Udhhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) lilizinduliwa rasmi mnamo Novemba 13, 2020 mjini Bagamoyo kwa lengo la kuboresha uhusiano baina ya wafanyakazi na uongozi wa Mamlaka ili kuongeza ari na ufanisi kazini.

Uzinduzi huo ulihudhuriwa na baadhi ya viongozi wa serikali wakiogozwa na Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Nishati Raphael Nombo ambaye alimwakilisha aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati Bi. Zena Said, Mwenyekiti wa Bodi, Menejimenti na wafanyakazi wa PURA pamoja na baadhi ya viongozi wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali na Afya (TUGHE) kwa ngazi za mkoa na taifa.

Akizungumza kabla ya kuzindua baraza hilo Bw. Nombo alieleza kuwa kuwa baraza hilo litakuwa jukwaa muhimu katika kuhakikisha kuna ushirikiano wa kutosha baina ya Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa PURA.

Alieleza kuwa ushirikiano huo utasaidia kuwezesha utendaji mzuri wa majukumu ya Mamlaka ambayo ni muhimu kwa maendeleo ya taifa kupitia sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia.

"Tunafahamu kuwa nia ya serikali katika kuanzisha mabaraza ya wafanyakazi ni kuwa na chombo kinachohakikishakuwahakinawajibu wa mwajiri na mtumishi vinapewa kipaumbele katika utekelezaji wa majukumu na huu ndio uwe msingi wa baraza hili kwenye Mamlaka hii muhimu" alieleza.



Bw. Nombo alifafanua kuwa baraza ni chombo chenye kuangalia maslahi ya pande zote mbili kwa manufaa ya taasisi na taifa kwa ujumla pamoja na kuibua hoja mbalimbali za kuongeza mafanikio ya taasisi.

"Hili ndilo jukwaa la kisheria la majadiliano ya pamoja kati ya viongozi na watumishi katika Utumishi wa Umma kuhusu wajibu na maslahi ya watumishi," aliongeza.

Vilevile alitoa wito kwa watumishi wa PURA kuhakikisha wanafahamu wajibu wao mahali pa kazi, wanatekeleza malengo yaliyopangwa katika muda uliopangwa.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PURA, Mhandisi Charles Sangweni alieleza kuwa kuwepo kwa baraza hilo la wafanyakazi wa Mamlaka hiyo kutaongeza kasi, ufanisi, na weledi katika kutekeleza majukumu ya Mamlaka kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Petroli ya mwaka 2015.

Alibainisha kuwa mabaraza ya wafanyakazi huanzishwa kisheria kwa madhumuni ya kuishauri serikali katika ngazi za idara zinazojitegemea, taasisi na wizara kuhusu usimamizi wa kazi na rasilimaliwatu, utekelezaji wa majukumu na kulinda haki na wajibu wa waajiri na wafanyakazi.

Aliongeza kwamba mabaraza hayo pia huanzishwa ili kutoa

ushauri kuhusu kujenga hali bora za kazi, maslahi ya wafanyakazi na kusimamia haki na ustawi katika sehemu za kazi.

"Wajibu wa mabaraza haya kama vyombo vya ushauri na usimamizi ni kuhakikisha kuwa waajiri na watumishi wanatambua wajibu na haki zao, pia wanazingatia maadili ya utumishi wao ili kuleta matokeo ya utendaji kazi wenye tija, staha na upendo," alifafanua.

Mhandisi Sangweni aliwataka viongozi na wawakilishi wa baraza hilo kufanya kazi kwa bidii huku wakimtanguliza Mwenyezi Mungu na wakizingatia nidhamu, uwajibikaji na uadilifu.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya PURA Profesa Gasper Mhinzi aliipongeza Mamlaka kwa hatua hiyo muhimu ya kuzindua Baraza la Wafanyakazi na kuwataki heri katika utendaji kazi wake.

Baraza hilo jipya la wafanyakazi PURA lina jumla ya wajumbe 34 ikihusisha wajumbe kutoka Menejimenti ya PURA ambao ni 13, wajumbe wa kuchaguliwa na wafanyakazi kutoka kila idara ambao ni nane, wengine ni wajumbe wa Halmashauri ya tawi la TUGHE ambao wako 11, mjumbe mmoja kutoka TUGHE mkoa na mjumbe mmoja kutoka Baraza Kuu la Wafanyakazi serikalini.

PURA yazindua Baraza la Wafanyakazi



Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya PURA, Profesa Gasper Mhinzi, Menejimenti na watumishi wa PURA wakiwa katika uzinduzi wa Baraza la Wafanyakazi la PURA. Aliyezindua baraza hilo ni Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Nishati Raphael Nombo. Wengine waliohudhuria hafla hiyo ni viongozi wa TUGHE kwa ngazi za mikoa na Taifa. Picha na Janeth Mesomapyia

PURA yaeleza fursa zilizopo kwenye sekta ya mafuta na gesi asilia

Na Janeth Mesomapyia

Kutokana na umuhimu uliopo katika ushiriki wa wazawa kwenye shughuli za maendeleo, timu ya wataalamu wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) walishiriki kwenye Maonesho ya Nne ya Mifuko na Programu za Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi jijini Arusha, ili kuongeza ufahamu kwa wananchi kuhusu fursa zinazopatikana katika sekta ndogo ya mafuta na gesi nchini.

Maonesho hayo yaliyofanyika katika Uwanja wa Sheikh Amri Abed kuanzia Februari 7 hadi 13, 2021 yaliandaliwa na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC).

Miongoni mwa fursa zinazopatikana kwenye shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli ni pamoja na ajira, usambazaji wa bidhaa na huduma za nyakula, usafi, ulinzi, uhandisi na nyinginezo.

Akizungumza na maandishi wa habari kwenye banda la PURA, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PURA Mhandisi Charles Sangweni alieleza kuwa moja ya kazi kuu za Mamlaka hii ni kuhakikisha wauzaji na watoa huduma wa ndani wanapewa kipaumbele katika kupata fursa zinazopatikana katika husika.

“Moja kati ya majukumu yetu kama Mamlaka, ni kuwajengea uwezo watanania wa kuzalisha na kutoa bidhaa na huduma za viwango vya juu ili kuwasaidia

kushindana na wenzao wa kimataifa, na kuweza kutumia fursa pindi zinapojitokeza” aliongeza.

Masuala mengine ambayo PURA ilianguzia ni pamoja na historia ya kuanzishwa kwa PURA na majukumu yake, shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi asilia, hali ya mikataba ya PSA na hali ya uzalishaji wa gesi asilia nchini.

Madhumuni ya maonyesho hayo kwa ujumla yalikuwa kukuza uelewa wa umma juu ya uwepo, majukumu na vigezo vilivyotumika katika kutoa huduma kwa fedha za uwezeshaji kuhamasisha raia kufaidika na fursa zinazopatikana katika mifuko hiyo.

Dhima ya maonesho hayo pia ilikuwa ni kujenga uelewa juu ya umuhimu wa kuweka akiba ya fedha na njia bora za kuwekeza katika miradi yenye faida kupitia uanzishaji na uimarishaji wa vikundi vya kifedha vya kijamii.

Maonesho hayo yalifunguliwa na Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa na kufungwa na Waziri wa Nchi (Sera, Uratibu, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Mhe. Jenista Mhagama.

Aidha wajasiriamali wadogo na wakati, wizara na taasisi za serikali, asasi za kiraia, taasisi za elimu na nyinginezo zilishiriki maonesho hayo yaliyohudhuriwa na mamia ya watu.



Wafanyakazi wa PURA na wadau kutoka kampuni za mafuta (kitaifa na kimataifa) kwenye kikao cha kujadili jinsi bora ya kuongeza ushiriki wa wazawa kwenye shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli. Kikao hicho kilifanyika ofisi za Makao Makuu ya PURA jijini Dar es Salaam. Picha na Janeth Mesomapyia

PURA yaeleza fursa zilizopo kwenye sekta ya mafuta na gesi asilia



Wafanyakazi wa PURA na wadau kutoka kampuni za mafuta (kitaifa na kimataifa) kwenye kikao cha kujadili jinsi bora ya kuongeza ushiriki wa wazawa kwenye shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli. Kikao hicho kilifanyika ofisi za Makao Makuu ya PURA jijini Dar es Salaam. Picha na Janeth Mesomapya

PURA yaimarisha ufuatiliaji wa utekelezaji wa shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli nchini



Timu ya wataalamu kutoka PURA hufika katika maeneo hayo angalau mara moja kila mwezi kwa lengo la kukagua masuala anuai yakiwemo yale ya kitaalamu, masuala ya usalama na afya mahala pa kazi, ushiriki wa wataanzania katika shughuli hizo na utekelezaji wa miradi ya uwajibikaji wa kampuni kwa jamii (Corporate Social Responsibility – CSR).“

Na Ebeneza Mollel

Katika kuhakikisha kuwa shughuli za mkondo wa juu wa mafuta na gesi asilia zinatekelezwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu zilizopo, PURA imeendelea kufanya kaguzi za mara kwa mara katika maeneo ambayo utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia unafanyika.

Timu ya wataalamu kutoka PURA hufika katika maeneo hayo angalau mara moja kila mwezi kwa lengo la kukagua masuala anuai yakiwemo yale ya kitaalamu, masuala ya usalama na afya mahala pa kazi, ushiriki wa wataanzania

katika shughuli hizo na utekelezaji wa miradi ya uwajibikaji wa kampuni kwa jamii (Corporate Social Responsibility – CSR).

Mbali na kuhakikisha kuwa shughuli zinatekelezwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu, PURA pia inahakikisha kuwa kampuni zinazofanya shughuli za utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini zinatekeleza majukumu yake kulingana na mpango kazi uliopitishwa na PURA.

Kwa mujibu wa Sheria ya Petroli ya mwaka 2015, moja ya jukumu la PURA ni kupitisha mpango kazi na bajeti ya kila kampuni na kuhakikisha kuwa kampuni hizo zinatekeleza

majukumu yaliyoainishwa katika mpango uliopitishwa.

Shughuli za utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi nchini zinaendelea katika maeneo mbalimbali nchini yakiwemo Songo Songo (Lindi), Mnazi Bay (Mtwara), Ruvu (Pwani) na Eyasi Wembere (Singida).

Aidha, hadi kufikia Machi, 2021 kiasi cha gesi asilia takribani futi za ujazo Trilioni 57.54 kimegunduliwa ambapo kati ya hizo, futi za ujazo Trilioni 10.46 kimegunduliwa nchi kavu na futi za ujazo Trilioni 47.08 kimegunduliwa maeneo ya bahari kuu. Bado mafuta hayajagunduliwa nchini ingawa tafti zinaendelea.

Mwongozo wa ushiriki wa watazania mbioni kukamilika

Na Ebeneza Mollel

Mamlaka ya Udhhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli imefanya kikao cha wadau kwa lengo la kupata maoni yao kuhusu mwongozo wa ushiriki wa watazania katika shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli (The Upstream Petroleum Local Content Guidelines).

Kikao hicho kilichofanyika tarehe 09 Februari, 2021 kwa njia ya mtandao kilileta pamoja zaidi ya wadau 40 wakiwemo kampuni za utafutaji, uendelezaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia nchini, taasisi za serikali, taasisi kutoka sekta binafsi na kampuni za utoaji huduma na ugavi wa bidhaa.

Katika kikao hicho, Mkuu wa Kitengo cha Ushiriki wa Wazawa na Ushirikishwaji Wadau kutoka PURA, Bw. Charles Nyangi, aliwasilisha rasimu ya Mwongozo ulioandaliwa na PURA.

Mwongozo huo ulijumuisha miongozo midogo midogo mitano ambayo ni: mwongozo wa uandaaji wa kanzidata ya kuwasajili watoa huduma, mwongozo wa kuandaa

mpango wa ushiriki wa Watazania, mwongozo wa kuchambua zabuni, mwongozo wa uwasilishaji wa taarifa za utekelezaji wa ushiriki wa watazania na mwongozo wa kushughulikia malalamiko yatakayojitokeza.

Mara baada ya kuwasilisha Mwongozo, wadau walipewa fursa ya kuuliza maswali na kuomba ufafanuzi. Aidha wadau walipata wasaa wa kutoa maoni, ushauri na mapendekezo. Miongoni mwa maswali yalioulizwa ni ulazima uliopo kwa watoa huduma kujisajili katika kanzidata, vigezo vitakavyotumika katika kusajili watoa kampuni za watoa huduma, na endapo kanzidata ya PURA na EWURA

itakuwa moja au zitakuwa kanzidata mbili tofauti.

Akifafanua baadhi ya hoja na kujibu baadhi ya maswali, Bw. Nyangi alieleza kuwa kanzidata ya watoa huduma itakuwa moja (kwa maana ya EWURA na PURA wameungana kuandaa kanzidata moja) ili kufanya wepesi kwa watoa huduma.

Aidha, kwa upande wa vigezo, Bw. Nyangi alidokeza kuwa kutakuwa na vigezo vya jumla ambayo kila mtoa huduma atakayehitaji kujisajili atatakiwa kuwa navyo na kutakuwa na vigezo mahususi kulingana na kazi husika. Aliongeza kuwa kwa sasa PURA kwa kushirikiana na wahitaji huduma ambao ni kampuni za utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi nchini inaandaa vigezo mahususi.

Kwa sasa PURA ipo katika hatua ya kuingiza maoni na mapendekezo yaliyotolea na wadau na kukamilisha kanzidata ya kuwasajili watoa huduma na wagavi wa bidhaa. Matarajio ni kuwa na mwongozo uliopitishwa kabla ya 30 Juni, 2021.



Kwa sasa PURA ipo katika hatua ya kuingiza maoni na mapendekezo yaliyotolea na wadau na kukamilisha kanzidata ya kuwasajili watoa huduma na wagavi wa bidhaa. Matarajio ni kuwa na mwongozo uliopitishwa kabla ya 30 Juni, 2021”.

PURA, wadau kuongeza ushiriki wa wazawa sekta ya mafuta na gesi

Na Janeth Mesomapya

Katika kuhakikisha ongezeko la ushiriki wa Watanzania katika shughuli za mkondo wa juu wa Petroli, Mamlaka ya Udhambi wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) imekutana na wadau wa sekta ya mafuta na gesi kujadili jinsi bora ya kufanikisha suala hilo.

Katika kikao hicho kilichofanyika hivi karibuni jijini Dar es Salaam, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PURA Mhandisi Charles Sangweni ameeleza kuwa moja ya majukumu ya Mamlaka hiyo ni kuhakikisha wazawa wanashiriki kikamilifu kwenye sekta ya mafuta na gesi kwa kuuza bidhaa na kutoa huduma pamoja kupata nafasi za ajira.

Aliongeza kuwa kufanikiwa kwa jukumu hilo kutategemea kwa kiasi kikubwa ushirikiano baina ya Mamlaka na wawekezaji wa sekta hiyo pamoja na wadau hao kufuata sheria na miongozo inayoelekeza jinsi ya Watanzania kushiriki katika sekta hiyo

Kwa upande wake Mkuu wa Kitengo cha Ushiriki wa Wazawa (Local Content & Stakeholders Engagement) Charles Nyangi alieleza kuwa lengo kuu la kikao hicho ni kuandaa vigezo ambavyo vitawezesha Watanzania kuuza bidhaa na kutoa huduma zenye ubora ili kukidhi mahitaji ya soko.

Alidokeza kuwa kwasasa PURA ikishirikiana na Mamlaka ya Udhambi wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) zinaandaa



Wafanyakazi wa PURA na wadau kutoka kampuni za mafuta (kitaifa na kimataifa) kwenye kikao cha kujadili jinsi bora ya kuongeza ushiriki wa wazawa kwenye shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli. Kikao hicho kilifanyika ofisi za Makao Makuu ya PURA jijini Dar es Salaam. Picha na Janeth Mesomapya

kanzidata (database) ambayo itatunza taarifa zote muhimu za Watanzania wanaotaka kushiriki kwenye sekta hiyo kwa kuuza bidhaa, kutoa huduma au kupata nafasi za ajira.



Lengo la kanzidata hii ni kuwa jukwaa la kukutanisha Watanzania watoa huduma na makampuni ya kimataifa ya mafuta na gesi yanayofanya uwekezaji nchini ambayo yanauhitaji wa bidhaa na huduma mbalimbali ambazo zinaweza kupatikana ndani ya nchi”.

“Lengo la kanzidata hii ni kuwa jukwaa la kukutanisha Watanzania watoa huduma na makampuni ya kimataifa ya mafuta na gesi yanayofanya uwekezaji nchini ambayo yanauhitaji wa bidhaa na huduma mbalimbali ambazo zinaweza kupatikana ndani ya nchi,” alisema

Nao wadau walioshiriki kikao hicho walitoa rai kwa Mamlaka kuhakikisha inaendelea kutoa elimu ya kuwawezesha Watanzania wengi zaidi kutumia fursa zilizopo kwenye tasnia hiyo kwa kuuza bidhaa na kutoa huduma bora na kuwapiku washindani wao wa nje ya nchi ili kujiongezea tija kiuchumi.

PURA, wadau kuongeza ushiriki wa wazawa sekta ya mafuta na gesi



Wafanyakazi wa PURA na wadau kutoka kampuni za mafuta (kitaifa na kimataifa) kwenye kikao cha kujadili jinsi bora ya kuongeza ushiriki wa wazawa kwenye shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli. Kikao hicho kilifanyika ofisi za Makao Makuu ya PURA jijini Dar es Salaam. Picha na Janeth Mesomapya

Waandishi wa Habari na Wahariri chachu ya uelewa wa shughuli za Mkondo wa Juu Wa Petroli kwa jamii

Na Janeth Mesomapyia

Takriban waandishi wa habari na wahariri 50 wa vyombo mbalimbali vya habari nchini wamekuwa sehemu ya warsha maalumu ya kuwaongezea uelewa wa shughuli za mkondo wa juu wa petroli nchini.

Warsha hiyo iliyoandaliwa na Mamlaka ya Udhhibiti Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) ilifanyika Desemba 17 na 18, 2020 katika Ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNICC) Posta, jijini Dar es Salaam.

Kwa kuzingatia umuhimu wa vyombo vya habari kwenye maendeleo ya sekta ndogo ya mafuta na gesi nchini, PURA iliandaa warsha hiyo kwa lengo la kuongeza uelewa kwa vyombo vya habari kuhusu Mamlaka na shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli.

Hii ililenga haswa kuwezesha vyombo vya habari kutoa taarifa mbalimbali za Mamlaka na shughuli zake, pamoja na sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia kwa wingi, usahihi na upana pamoja na kuboresha uhusiano kati ya Mamlaka husika na vyombo vya habari.

Akiwasilisha mada ya uanzishwaji wa PURA na majukumu yake kwenye siku ya kwanza ya warsha hiyo, Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PURA wa Mamlaka Mhandisi Charles Sangweni aligusia masuala mbalimbali ikiwemo historia ya usimamizi wa shughuli za utafutaji na uzalishaji wa mafuta nchini.

“Shughuli za utafutaji

wa mafuta nchini zilianza mwanzoni mwa miaka ya 1950, ambapo mwaka 1974 gesi asilia iligunduliwa kisiwani Songo Songo. Hadi sasa kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa nchini ni futi za ujazo trilioni 57.54,” alieleza.

Mha. Sangweni alizungumzia pia uanzishwaji wa PURA mnamo mwaka 2005 baada ya kupitishwa Sheria ya Petroli, muundo wa taasisi na majukumu yake pamoja na mafanikio yaliyopatikana hadi sasa.

Alieleza kuwa baadhi ya mafanikio yaliyofikiwa hadi sasa ni pamoja na kuimarika kwa mifumo ya kisheria na udhibiti (Legal and Regulatory framework) katika uendeshaji wa sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia na kuongezeka kwa ushiriki wa Wazawa katika shughuli za mkondo wa juu wa petroli.

“Mafanikio mengine ni kuimarika kwa shughuli za kaguzi za gharama katika mikataba ya PSAs (PSA Audit), iliyopelekea kuokoa fedha zaidi ya shilingi bilioni 20 hadi sasa,” aliongeza.

Kwa upande wake Mjiolojia kutoka PURA, Bw. Faustine Matiku aliyewasilisha mada ya hali ya tasnia ya mafuta na gesi nchini

Mada hii iligusia masuala mbalimbali ikiwemo dhana za jiolojia ya petrol, shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli, maeneo yenye uwezekano wa kupatikana mafuta na gesi asilia Tanzania na historia ya utafiti wa mafuta nchini.

Mengine ni visima virefu vya utafiti wa mafuta vilivyowahi kuchimbwa nchini, njia mbalimbali za usafirishwaji wa gesi asilia na mradi wa usindikaji

wa gesi asilia kuwa kimiminika (LNG)

Naye Mkuu wa Kitengo wa ushiriki wa watazania na ushirikishwaji wa wadau (Local Content & Stakeholders Engagement) Bw. Charles Nyangi alifafanua maana ya ushiriki wa watazania na ushirikishwaji wa wadau kwenye sekta ya mafuta na gesi, maeneo ya kipaumbele kwenye ushiriki wa wazawa ikiwa ni pamoja na kuwawezesha watazania kuzalisha bidhaa na kutoa huduma bora, kuongeza nafasi za ajira na kuongeza uwezo katika mnyororo wa thamani kwenye shughuli za mkondo wa juu wa petroli.

Maeneo mengine aliyoyagusia ni sera, miundo ya kisheria na kimamlaka inayoongoza masuala ya ushiriki wa wazawa, ushiriki wa wazawa nchini Tanzania bidhaa na huduma zinazotolewa na watoa huduma wazawa nchini Tanzania, mafanikio ya PURA katika kuhamasisha ushiriki wa wazawa, changamoto, uhamasishwaji wa wazawa kushiriki katika sekta ya mkondo wa juu wa petrol na ugawanaji wa kinachozalishwa kwenye sekta ndogo ya mafuta na gesi asilia.

Warsha hii ilikuwa ya mafanikio kwani waandishi na wahariri hao waliongeza uelewa wa shughuli za mkondo wa juu wa petroli na hatimaye kutoa taarifa mbalimbali kwa umma wa watazania kuhusu sekta ndogo ya mafuta na gesi kupitia vyombo vyao vya habari husika.

Waandishi wa Habari na Wahariri chachu ya uelewa wa shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli kwa jamii



Waandishi wa Habari na Wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari nchini wakiwa kwenye warsha iliyoandaliwa na PURA jijini Dar es Salaam. Warsha hiyo ilikuwa na lengo la kuongeza uelewa wa shughuli za Mkondo wa Juu wa Petroli kwa umma kupitia vyombo vya habari. Picha na Janeth Mesomapya.

PURA katika mapinduzi ya kiuchumi

Na Hafidh Kido

Mara kwa mara katika hotuba zake Rais Dk. John Magufuli alikuwa akikariri maneno ya kuonyesha anahitaji Watanzania wanufaike na rasilimali zao hasa madini na gesi asilia.

Anasema, sisi si masikini kwa kuwa tuna vitu ambavyo wengi hawajapewa na pengine ndiyo sababu baadhi ya mataifa ya kimagharibi hayavutiwi na maendeleo yanayopatikana nchini, wanasababisha chokochocho za kutuvuruga.

Mwaka 2019 Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani akiwa katika kongamano la siku tatu la kuhamasisha uwezeshaji na uwekezaji katika shughuli za utafutaji na uchimbaji mafuta na gesi asilia alisema Tanzania imefungua mikono yake kuwataka wawekezaji waje kwa kuwa rasilimali hiyo ipo kwa wingi.

Aidha, kongamano hilo lililofanyika kuanzia Oktoba 2-3, 2019 jijini Dar es Salaam, lilihudhuriwa na watu zaidi ya 500 kutoka mataifa 67 duniani.

"Kila mmoja ni shahidi, mafanikio ya sekta ya gesi hivi sasa yameongezeka ambapo mwaka 2018, gesi ilichangia asilimia 2 ya pato la taifa, kutoka asilimia 0.9 mwaka 2017, ongezeko hili pia linatokana na kazi ya usambazaji na uzaji wa gesi hiyo kutoka

kwenye uzalishaji kwenda kwa watumiaji, hakika haya ni mafanikio makubwa."

Aliongeza kuwa matumizi ya gesi yameongezeka kutoka kipimo cha ujazo wa gesi futi Milioni 45(mmsf) mwaka 2013/14 , hadi kufikia Milioni 110 mwaka 2019 kwa ajili ya

kuzalisha umeme, pia futi za ujazo takribani Milioni 70, zinatumiwa kwa ajili ya matumizi mengine ya ndani ikiwepo katika magari pamoja na viwanda.

Kwa miaka 15 iliyopita hadi sasa, Matumizi ya gesi ni takribani asilimia 1 ya kipimo cha ujazo wa Trilioni 57.54 ya gesi yote iliyogunduliwa nchini, matumizi hayo yanaendelea kuongezeka kutokana na kuwepo na miundombinu ya kuzalisha umeme unaotumia gesi, pamoja na mahitaji ya matumizi mengine ya gesi kuongezeka.

Alisema bado shughuli za utafiti zinaendelea ili kupata gesi nyingi zaidi kwa matumizi ya Watanzania katika miaka ijayo.

Takribani asilimia 55 ya umeme unaotumika nchini unazalishwa kwa kutumia rasilimali ya gesi. Matumizi ya gesi ni nafuu kwa asilimia 40 ya matumizi ya kuni na mkaa na kuhifadhi mazingira, takribani magunia 5,000 ya mkaa hutumiwa kila mwaka kwa mkoa wa Dar es salaam pekee, hivyo gesi hiyo itachangia kwa kiasi kikubwa katika utunzaji wa

mazingira.

Hivi karibuni Mamlaka ya Udhhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), ilifanya warsha kwa wanahabari na wahariri kuzungumza nao na kujadiliana juu ya hali ya rasilimali hiyo nchini, ambapo miongoni mwa watoa mada alikuwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PURA, Mhandisi Charles Sangweni aliyewapitisha wanahabari katika historia ya utafutaji mafuta na gesi asilia nchini, alisema:

"Shughuli za utafutaji mafuta na gesi asilia nchini zilianza mwaka 1952 kupitia Kampuni ya Agip kutoka Italia. Licha ya shughuli hizo kuanza mwaka huo, Kampuni ya Agip ilifanya ugunduzi wa kwanza katika Kisiwa cha Songo Songo(Lindi) mwaka 1974 ambao ulifuatiwa na ugunduzi mwingine katika eneo la Mnazi Bay (Mtwara) mwaka 1982.

"Hata hivyo, gesi asilia hiyo haikuendelezwa kwa kuwa ilionekana haina manufaa ya kiuchumi (uneconomical) kwa wakati huo. Baada ya ugunduzi huo, Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) liliendelea kufanya utafiti ikiwa ni pamoja na kuchimba visima mbalimbali kwa ajili ya kuthibitisha kiasi cha gesi asilia kilichopo katika maeneo ambako gesi asilia iligunduliwa. Hadi Novemba, 2014 kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa nchini ni futi za ujazo trilioni 53.28."

PURA katika mapinduzi ya kiuchumi

Mhandisi Sangweni alibainisha, hadi sasa kiasi cha gesi asilia kilichogunduliwa nchini ni futi za ujazo trilioni 57.54, ambacho kinaweza kutumika kwa miaka mingi zaidi na kukumbusha kuwa kinachotumika kwa sasa ni asilimia ndogo tu ya utajiri uliopo ardhini na majini.

Akizungumzia uanzishwaji wa PURA, Mhandisi Sangweni alisema mamlaka hiyo iliundwa kupitia kifungu namba 11, cha Sheria ya Petroli ya mwaka 2015.

“Sababu za uanzishwaji wake ni pamoja na ugunduzi mkubwa wa gesi asilia kwenye kina kirefu cha bahari. Uhitaji wa uimarishaji wa mifumo ya kisheria, kitaasisi na udhibiti. Kutenganisha majukumu ya kibiashara na udhibiti wa sekta ya petroli nchini na kuendana na mabadiliko ya mfumo wa uendeshaji na usimamizi wa sekta ya mafuta duniani,” alisema Mhandisi Sangweni na kufafanua:

“Majukumu ya PURA yameainishwa katika Sheria ya Petroli ya 2015, kifungu Na. 12 na kwa ujumla wake yamegawanyika katika makundi makuu matatu ikiwemo: kuishauri Serikali juu ya masuala mbalimbali yahasuyo Utafutaji, Uendelezaji na Uzalishaji wa mafuta au gesi asilia;

“Kusimamia na kudhibiti shughuli zote zinazohusiana na mkondo wa juu wa petrol; na kusimamia utekelezaji wa mradi wa kuchakata gesi asilia kuwa

katika mfumo wa kimiminika (Liquefied Natural Gas Project). Ambapo majukumu haya yameainishwa zaidi kwenye kifungu cha 12 (2), ambapo yanazalisha majukumu 18 kwa ujumla wake.”

Kwa mujibu wa taarifa ya utekelezaji wa ujenzi wa miundombinu ya gesi asilia kutoka Madimba-Mtwara, Songo Songo – Lindi na Pwani hadi Dar es Salaam ya Machi, 2015 inaeleza kuwa Tanzania imeamua kutumia gesi asilia kuzalisha umeme kwa sababu mbalimbali ikiwamo;

Kupunguza utegemezi wa umeme unaozalishwa kwa kutumia maji (Hydropower) ambao unaathiriwa na mabadiliko ya tabianchi kama ukame, vilevile kupunguza matumizi ya fedha za kigeni zinazotumika kuagiza mafuta kutoka nje kwa ajili kuzalisha umeme.

Sababu nyingine ni kushirikisha sekta binafsi katika sekta ya nishati na kuvutia

wawekezaji katika shughuli za utafutaji mafuta na gesi asilia nchini.

Ambapo, imebainika utekelezaji wa mradi huu utaiwezesha nchi kupata umeme wa uhakika na wa bei nafuu.

Itakapokamilika miundombinu hiyo itaokoa zaidi ya Dola za Marekani Bilioni 1 sawa na shilingi Trilioni 1.6 kwa mwaka, zinazotumika sasa kuagiza mafuta kwa ajili ya kufua umeme kwa kutumia mitambo ambayo tayari ipo nchini.

Kadhalika mitambo mipya inayojengwa itapata gesi asilia kuzalisha umeme wa bei nafuu.

Aidha, hadi sasa Shirika la Umeme TANESCO kupitia gridi ya taifa inazalisha Megawati 1,565.72 na umeme utokanao na gridi ya taifa na vyanzo vilivyo nje ya gridi ni Megawati 1,601.84, ambapo asilimia 86.5 ya umeme unaozalishwa nchini unamilikiwa na Tanesco.

Hii ni mbali ya Megawati 2115 zitakazozalishwa baada ya kukamilika mradi mkubwa wa Julius Nyerere (JNHPP). Mahitaji kwa sasa ni Megawati 1,177.20.

Aidha, umeme unaozalishwa kwa kutumia gesi asilia nchini ni zaidi ya asilimia 57 ya umeme wote unaozalishwa.



**Umeme
unaozalishwa
kwa kutumia gesi
asilia nchini ni
zaidi ya asilimia
57 ya umeme wote
unaozalishwa.**

Wanafunzi, wanagenzi watembelea mitambo ya uzalishaji gesi asilia

Na Janeth Mesomapyia

Timu ya wafanyakazi wa Mamlaka ya Udhhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) hivi karibuni wameongoza jopo la wanafunzi wa mafunzo kwa vitendo na wanagenzi (interns & field students) kwenye Mamlaka hiyo kutembelea miradi na mitambo mbalimbali ya uzalishaji na uchakataji wa gesi asilia mkoani Mtwara na Lindi.

Katika ziara hiyo wanafunzi hao wamepata fursa ya kutembelea mradi wa kupokea gesi asilia Kinyerezi (GRF), Kisima cha Mkuranga 1, eneo la uzalishaji gesi asilia Mnazi Bay, mitambo ya kuchakata gesi asilia Madimba na mitambo ya kupokea gesi Mtwara.

Jopo hilo pia lilitembelea maeneo ya kijiolojia (geological sites) sita na maeneo mawili yenye mvujo wa mafuta (oil seep) ya Wingayongo na Makukwa.

Kwa mujibu wa kiongozi wa

ziara hiyo, Mjiolojia Faustine Matiku ziara hiyo ilikuwa na lengo law kuwaonyesha kwa vitendo wanafunzi hao kazi ambazo PURA inafanya na miradi ambayo inaidhibiti kwa mujibu wa sheria.

“Timu hii ilikuwa pia na wanafunzi wasio na taaluma za jiolojia na uhandisi wa petroli hii ilikuwa ni kuwawezesha kupata uelewa wa shughuli za utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi asilia,” alieleza.

Akizungumzia maeneo ya kijiolojia yaliyotembelewa, Mjiolojia wa Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) Adam Sajilo ameeleza kuwa wanafunzi hao wameona miamba inayopatikana kwenye pwani ya kusini mwa Tanzania na kujifunza aina zake na jinsi ilivyotengenezwa.

“Wameweza hata kujifunza kuwa hata miamba ina umri na unaweza kujua umri wa mwamba fulani kwa kuangalia viumbe walio kwenye mwamba husika,” aliongeza.

Mwanagenzi Mjiolojia Bahati Mohamed ameeleza kuwa ziara hiyo imekuwa ya manufaa kwake kwani amefanikiwa kuona kwa macho vitu ambavyo vinatengeneza rasilimali za mafuta na gesi ardhini.

Kwa upande wake, Naomi Mwakibolwa ambaye ni mwanafunzi wa mwaka wa nne wa Shahada ya Uhandisi wa Petroli katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam ameeleza kuwa ziara hiyo imemsaidia kuhusianisha vitu alivyofundishwa darasani na uhalisia wake kiutendaji kwenye maeneo ya uzalishaji.

Naye Mwanagenzi wa kada ya Manunuzi Winston Kayona amesema ziara hiyo imemsaidia kujifunza umuhimu wa mchakato wa manunuzi katika kuleta maendeleo kwenye mnyororo wa thamani wa sekta ya mafuta na gesi.



Wanafunzi, wanagenzi watembelea mitambo ya uzalishaji gesi asilia



Wanafunzi wa mafunzo kwa vitendo na wanagenzi kutoka PURA wakiwa kwenye ziara ya kutembelea miradi na mitambo ya uzalishaji na uchakataji wa gesi asilia mkoani Mtwara na Lindi. Maeneo waliyotembelea ni pamoja na mradi wa kupokea gesi asilia Kinyerezi (GRF), Kisima cha Mkuranga 1, eneo la uzalishaji gesi asilia Mnazi Bay, mitambo ya kuchakata gesi asilia Madimba, mitambo ya kupokea gesi Mtwara na maeneo ya kijiolojia sita. Picha na Janeth Mesomapy

Wanafunzi, wanagenzi watembelea mitambo ya uzalishaji gesi asilia



Wanafunzi wa mafunzo kwa vitendo na wanagenzi kutoka PURA wakiwa kwenye ziara ya kutembelea miradi na mitambo ya uzalishaji na uchakataji wa gesi asilia mkoani Mtwara na Lindi. Maeneo waliyotembelea ni pamoja na mradi wa kupokea gesi asilia Kinyerezi (GRF), Kisima cha Mkuranga 1, eneo la uzalishaji gesi asilia Mnazi Bay, mitambo ya kuchakata gesi asilia Madimba, mitambo ya kupokea gesi Mtwara na maeneo ya kijiolojia sita. Picha na Janeth Mesomapya